

Swahili transcript:

Nchi ya Tanzania ina vivutio vingi hasa kwa watalii. Tuna mbuga za wanyama kama vile Serengeti, Ngorongoro, Manyara, Mikumi, na pia tuna hifadhi za taifa kama hifadhi ya Selous, kuna hifadhi pia ya mto Ruaha pamoja na vivutio vingine. Na katika kila mwaka, watalii wengi kutoka sehemu mbalimbali duniani wanakuja Tanzania, kuja kutembelea na kujionea mandhari nzuri ya nchi hii ya Tanzania. Wanakuja kutembelea hizi mbuga za wanyama. Wanatembelea pia vivutio vingi ambavyo viko Tanzania. Pia vilevile watalii wengi wanapenda kwenda kupanda mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro uko Tanzania na uko katika mkoa wa Kilimanjaro, ni kaskazini mwa Tanzania. Kwa hiyo watalii wengi wanapenda kuja Tanzania pia kuja kuuona mlima Kilimanjaro na kuupanda pia. Kwa sababu mlima Kilimanjaro ni mlima mrefu katika bara la Afrika, na vilevile ni mlima wa tatu kiurefu katika dunia. Kwa hiyo watalii wengi wanakuja pia kuuona mlima huu na kupanda. Vilevile kuna vivutio vingi sana ambavyo watalii wengi wanapendelea na wengi ambao wanapendelea kwenda mkoa wa Arusha kuna hili kabila la wamasai, watu wa kabila la wamasai pia watalii wengi wanapenda kwenda kuwaona kutokana na taratibu zao na desturi zao za maisha yao ya kila siku. Ninawapenda sana wamasai kwa sababu wao wana taratibu zao ambazo ziko tofauti kidogo na watanzania wengine au na makabila mengine. Ninapenda desturi zao, jinsi wanavyovaa nguo zao, wao wana nguo zao ambazo ni maalum, pia wana urembo ambao wanautumia kuvaa, ambao ni tofauti na watanzania wengine. Pia kabila la wamasai limekuwa ni kivutio kikubwa kwa watalii na hata watanzania wenyewe.

English translation:

In Tanzania, we have so many tourist attractions. We have national parks like Serengeti National Park, Ngorongoro National Park, Manyara National Park, and Mikumi National Park. We also have national reserves like Selous, Ruaha River Reservation, and others. Every year, many tourists from different parts of the world come to Tanzania to visit this

beautiful country. They also visit these national parks and other tourist attractions that are found in Tanzania. Most of them come to see and climb Mount Kilimanjaro. Mount Kilimanjaro is in the northern part of Tanzania, in a region called Kilimanjaro. Mount Kilimanjaro is the largest mountain in Africa; it is also the third largest mountain in the world. So many tourists come to Tanzania not only to see Mount Kilimanjaro, but also to climb it. The Maasai tribe is one of the major tourist attractions in Tanzania, just because of their culture, traditions and customs. These people are found in the Arusha region, and many tourists go there to see these people and learn from them. I like Maasai people because of their unique way of life, which is different from other Tanzanian tribes. I like the way they dress, because they have their own unique dresses. They also design their own bangles, necklaces and earrings which are unique and beautiful. So the Maasai tribe has been a major tourist attraction even to Tanzanians.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated